JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## WITO WA KUSHIRIKI KATIKA MPANGO WA KUWAUNGANISHA VIJANA KATIKA UONGOZI (GENERATION CONNECT YOUNG LEADERSHIP PROGRAMME)

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania(TCRA) inapenda kuutarifu umma kuwa Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) linawaalika Vijana kushiriki mpango maalumu wa uongozi wa Kidijitali uitwao Generation Connect Young Leadership Programme (GCYLP). Mpango huu unalenga kuwawezesha vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 28 kuwa viongozi katika ulimwengu wa teknolojia.

Mpango huu unatoa fursa kwa washiriki 30 kila Mwaka na kuwapatia mafunzo, ushauri (mentorship), na ufadhili ili kutekeleza miradi bunifu ya maendeleo ya kidijitali katika jamii zinazowazunguka. Washiriki hupokea ruzuku kwa miradi yenye tija na athari chanya pamoja na fursa za kujenga mitandao ya kimataifa na kushiriki katika matukio mbalimbali duniani.

Maelezo zaidi yanapatikana kupitia kiunganishi hiki:
**https://www.itu.int/generationconnect/empower/generation-connect-young-leadership-programme-in-partnership-with-huawei-v2/itu-generation-connect-young-leadership-programme-2026-2027-frequently-asked-questions/.**

TCRA inawahamasisha wadau wote, wakiwemo wanafunzi, wabunifu na wajasiriamali chipukizi kushiriki katika mpango huu.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 31 Machi, 2026. Tafadhali jisajili kupitia kiunganishi hiki:
**https://www.itu.int/generationconnect/empower/generation-connect-young-leadership-programme-in-partnership-with-huawei-v2/**.

Imetolewa tarehe **24 Machi, 2026.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Tue Mar 24 21:23:41 EAT 2026

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz